

Mradi wa kukomesha ajira kwa watoto wazinduliwa

Na Mwandishi Wetu

Dar es Salaam

WAZIRI wa Kazi na Ajira, Gaudensia Kabaka, amezindua kampeni ya kukomesha ajira kwa watoto katika mashamba ya tumbaku yaliyoko Wilaya za Urambo na Sikonge, Tabora.

Uzinduzi huo ulifanyika Dar es Salaam na kuhudhuriwa na maofisa wa taasisi zinazojihusisha na ukomeshaji wa ajira hizo katika mashamba hayo.

Taasisi hizo ni PROSPER, Winrock

International, TAWLAE na TDFT ambazo zitashiriki katika kampeni hiyo ya miaka mitano hadi 2015.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Waziri Kabaka alisema Serikali itakuwa mstari wa mbele kushirikiana na taasisi hizo katika mapambano dhidi ya vita hivyo.

Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimesaini mikataba ya kimataifa ya kudhibiti ajira kwa watoto, kwa hivyo, hatuko tayari kuona watoto wakiendelea kuajiriwa katika mashamba hayo na mengine bila sisi kuchukua hatua.

"Tutaiunga mkono PROSPER kwa sababu katika shughuli hii, wao wana nafasi kubwa kwa sababu watakuwa wakitoa fedha kwa akila familia zenye watoto wao na watoto husika watapelekwa shule ili nao wapate elimu kama wenzao," alisema Waziri Kabaka.

Kwa mujibu wa Waziri Kabaka, PROSPER itatoa elimu katika jamii wilayani Sikonge na Urambo pamoja na Dola 150 za Marekani kila mwaka katika kila familia ambapo Dola 40 kati ya hizo zitakuwa ni kwa ajili ya masomo ya watoto wanaofanya kazi katika

mashamba hayo.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya PROSPER, Mary Kibogoya, alisema wakati wa shughuli zao watawaelimisha wananchi umuhimu wa kuwa na mazao mbadala kwa vile uzoefu unaonyesha watoto hao wanajingiza katika kazi hizo baada ya kukosa kilimo kingine.

Alisemapiakwamba, watawaelimisha wazazi na wananchi kwa ujumla njia za ujasiliamali kwa kuwa kama watakuwa wajasiliamali kasi ya watoto kufanya kazi katika mashamba ya tumbaku itapungua.